UMOJA WA WANAWAKE MAKANISA YA WABATISTI

Wafanya Kazi pamoja na Mungu

1 Kor. 3:9

MAANA SISI TU WAFANYA KAZI

PAMOJA NA MUNGU

I WAKORINTHO 3:9

# KITABU CHA MAELEZO

## Umoja wa Wanawake Waenezao Injili

© Copyright, 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
P.O. BOX 30370
NAIROBI, KENYA

# YALIYOMO

**Dibaji**

*Sura ya 1*--**KUJIFUNZA JUU YA UMOJA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI** ........................... 7

*Sura ya 2*--**SHABAHA ZETU NA VILE TUNAVYOZIFIKIA** 16

*Sura ya 3*--**VIONGOZI NA WASHIRIKI NA KAZI YAO** .. 27

*Sura ya 4*--**WANAWAKE WABATISTI WAJIUNGA PAMOJA** ........................................ 32

**VIFUNGU VYA BIBLIA KUJIFUNZA NA KUKUMBUKA** 36

## DIBAJI

Wanawake ambao wanampenda Kristo wanataka kushiriki upendo huu pamoja na wengine. Katika Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili, wanawake wana nafasi hii ya kujifunza kushuhudia.

Kitabu hiki, *Kitabu cha Maelezo,* yaani 'handbook', ambacho kilitayarishwa na Bi. Carter, kitakuwa kiongozi katika kazi hii. Wakati unapokisoma kitabu hiki, utafahamu kusudi na shabaha za Ushirika. Utaweza kujifunza kazi ya kila kiongozi na mshiriki, utajua kwamba makundi m'engine ya wanawake pande zote za ulimwengu wanashirikiana Injili.

Ni ombi letu kwamba utajaribu kufanya vizuri katika kundi lako. Kwa njia hii tutatimiza kusudi letu 'wafanya kazi pamoja na Mungu.'

Mwandishi anataka kuwashukuru washiriki wa Komiti ya Kazi ya Wanawake ambao walisaidia katika kukitayarisha kitabu hiki. Hawa ni Bi. Boyd Pearce, Bi. David Whitson, Bi. Frank Baugh, na Bi. Helen Gilmore. Shukrani vile vile kwa wafuatao waliosaidia katika kusoma maandiko kabla ya kuchapwa na kufanya madokezo: Bi. Ralph Harrell, Bi. Al Cummins, na Bi. Dot Emmons.

# KUJIFUNZA JUU YA UMOJA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

## MWANZO WETU

Tangu wakati ule makanisa ya Kibatisti yalipoanzishwa katika Afrika ya Mashariki, wanawake katika makanisa hayo walitafuta njia ambayo wangeweza kumtumikia Bwana na kufanya kazi yake ya kushiriki habari njema ya wokovu. Kwa hiyo, chama hiki kilitungwa, ambacho kwa sasa chaitwa 'Umoja wa Wanawake Waenezao Injili.' Kilizaliwa moyoni mwa wanawake ili wawe 'Wafanya kazi pamoja na Mungu.' Na wanawake wafanya kazi pamoja kueneza habari njema za Mwokozi wetu na kuendelea kukua kwa upendo wa Bwana.

Kama vile tulivyosoma katika Biblia zetu, tumepata kujua jinsi wanawake walivyokuwa wafanya kazi pamoja katika Agano Jipya. Sisi tumeona kwamba wanawake walikuwa na upendo, wakaabudu pamoja na kumtumikia Kristo, tena ya kwamba Kristo akapendezwa na kazi yao na hata akawasifu kwa sababu yake.

* Mwanamke ndiye aliyekuwa *Mama ya Yesu.* Yesu, Mwokozi wa ulimwengu wote, alizaliwa na bikira, Mariamu.

* Wanawake *waliwakaribisha wahubiri.* Nyumba moja iliyokuwa wazi sikuzote kwake Yesu ni ile ya Martha na Mariamu. Naye Lidia, mwanamke Mkristo mfanya biashara, alimkaribisha Paulo pamoja na wenzake alipokuwa akihubiri katika ule mji aliokaa. Na katika Korintho, nyumba yao Prisila na Akila ilikuwa wazi kwake Paulo.

* **Wanawake *walisaidia katika kuwazika waliokufa.***

* Wanawake *walifungua nyumba zao kuwa mahali pa kukutanikia kwa ajili ya'kumwabudu Mungu na kulisoma Neno la Mungu.*

* *Wanawake waliwafundisha vijana nyumbani.* Timotheo alikua katika nyumba ya Kikristo. Eunike alikuwa mama yake Timotheo naye Loisi alikuwa Bibi yake.

* Wanawake walisaidia hao ambao hawakujiweza. Dorkasi alikuwa mfano mwema hapa, alipokuwa akisaidia kwa kuwashonea wengine nguo na kufanya vitendo vyema.

* Pia *wanawake walitoa mali yao.* Mfano mzuri sana ni ule wa kutoa dhabihu ambao umeandikwa juu ya yule mwanamke mjane aliyekuwa maskini. Alitoa yote aliyokuwa nayo.

* *Wanawake walifanya kazi kanisani.* Fibi alikuwa shemasi kanisani.

## KUSUDI LETU

Kusudi letu hasa ni kushiriki ujumbe ule wa wokovu; kudhihirisha maisha ya Kikristo nyumbani na katika jamii; kusoma Biblia; kuomba peke yetu na pamoja na jamaa zetu; kutoa zaka zetu na sadaka zetu; kuwatumikia wengine na kueneza Injili katika Afrika ya Mashariki yote na dunia yote.

## KIFUNGU CHA KUTUONGOZA CHA DAIMA

*'Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu'*

*1 Wakorintho 3:9*

# WIMBO WETU


## NATAKA NIMJUE YESU

1. Nataka nimjue Yesu, Na nizidi kumfahamu,
Nijue pendo lake, na Wokovu wake kamili.
   Zaidi, zaidi, nimfahamu Yesu,
   Nijue pendo lake, na Wokovu wake kamili.
2. Nataka nione Yesu, Na nizidi kusikia
Anenapo Kitabuni, Kujidhihirisha kwangu.


3. Nataka nifahamu, na Nizidi kupambanua
Mapenzi yake, nifanya, Yale yanayompendeza.

4. Nataka nikae naye, Kwa mazungumzo zaidi,
Nizidi kuwaonyesha, Wengine wokovu wake.

*Key Ab 6/8*



# MFANO WETU




Ule mfano ni umbo la kichwa maradufu cha samaki, dalili ambayo ina maana kuu kwa vile ilivyotumiwa sana katika siku za kwanza za Ukristo. Wafuasi wa Kristo, waliogopa mateso wakivumbuliwa, hawakuonyesha imani yao kwa adui zao. Ilikuwa desturi yao kufanya ishara ya kichwa cha samaki walipokutana na mtu ambaye hawakumjua yeye kuwa Mkristo. Ikiwa mtu alikuwa adui ya Ukristo, alama haikuwa na maana kwake. Ikiwa angekuwa mwenye imani, angetambua alama na kutambuliwa kama rafiki.

Dalili ya samaki ilitumiwa na Wakristo wa kwanza kwa kuwa katika lugha ya Kigiriki herufi za kwanza za jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Mwokozi, herufi zilitumiwa kuandika neno lile samaki. Kwa hiyo dalili hii ilikuwa ya muhimu kwa Wakristo kama ukiri wa imani yao kwa uungu wa Kristo.

Kandokando ya ncha za mfano imeandikwa: Umoja wa Wanawake, Makanisa ya Wabatisti. Katikati pana picha ya Biblia, hali imefunguliwa 1 Wakorintho 3:9.... "wafanya kazi pamoja na Mungu,' ambayo ni maneno ya kuongoza Umoja wa Wanawake Waenezao Injili.

Juu ya Biblia iliyo wazi mwenge wenye nuru, dalili ya Mwokozi aliyesema: 'Mimi ndimi nuru ya ulimwengu: yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.' Nguzo za mwenge, iliyoonekana nyuma na chini ya mfano wa dunia, inatoa shauri ya uwezo wa kutia nguvu, utunza, na wokovu wa Mungu, Baba yetu, ambaye pendo lake liko juu, chini na nyuma yetu tukifuata Nuru ya Uzima. Mfano huu unatoa shauri ya kwamba hakuna mpaka wa Injili.

Mfano huu ambao umeandikwa kwa lugha nyingi unatumiwa na wanawake wa 'Umoja wa Wanawake Waenezao Injili' katika nchi nyingi.

## WIMBO JUU YA MFANO WETU

## TANGU WAKATI ULE

1. Tangu wakati ule,
Makanisa ya Kibatisti,
Tulipoyaanzisha,
Ulimwengu pote.

Tuliunda chama Umoja wa Wanawake
Waenezao Injili,
Pamoja na Mungu.

2. Mfano huu ni umbo,
Kama kichwa cha Samaki,
Wafuasi Wakristo,
Walipoutumia.

3. Kichwa hiki cha Samaki,
Kilikuwa ishara,
Kwa Wakristo wakikutana,
Na mtu safarini.

4. Huyo Mwana wa Mungu,
Yesu Kristo Mwokozi,
Kwa lugha ya Kigiriki,
Ndiyo neno Samaki.

5. Basi sote Wanawake,
Tushikane pamoja,
Tuwafanyi kazi,
Pamoja na Mungu.

**Key C 4/4**

|d: –.m |s: s | l: l |s: – | d: –.m |s.s: f | m.f: m |r: – |

|d: –.m |s: s | l: l |s: – | d: –: d |r: m | r: r |d: – |

|d' : –.d' |t: l | s: – |m: –.l | s: f.m |f: m.r | r: – |–: – |

|d: –.m |s: s | l: l.l |s: – |d: –.d |r: m | r: – |d: – |

Umetungwa na Priscilla Timothy

## VITABU VYETU

Maandiko hutuongoza katika mipango yetu yote. Mipango yetu hutolewa katika kitabu ambacho huchapwa baada ya kila miezi mitatu kiitwacho *'IWE NURU.'* Maandiko haya ni ya kutuongoza katika kuisoma Biblia, Uenezaji wa Injili, na maisha ya Kikristo. *Kitabu cha Maelezo'* ni kitabu cha kutusaidia katika maongozi ya mipango yetu kwa kila kundi. Nacho kitabu chetu chenye maongozi makuu ni Biblia. 'Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko.' (Mathayo 22:29.) Mpango wa kuisoma Biblia kila siku waweza kupatikana katika kurasa za mwisho za Kitabu cha Shule ya Jumapili, *'Masomo.'* Vitabu hivi vyapatikana kutoka kwa Baptist Publications House, Box 30370, Nairobi, Kenya.

## VYAMA VYETU

**Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili** ni chama cha wanawake wa makanisa ya Kibatisti. Imewapasa wanawake wote wa kanisa kuwa washiriki wa chama hiki. Wanawake wengine vile vile wanaweza kukaribishwa kujiunga katika chama hiki.

**Umoja wa Wanawake Waenezao Injili** ni chama cha wanawake Wabatisti katika jumuiya au taifa. Kimefanywa na shirika zote kutoka katika makanisa ya Kibatisti ya sehemu fulani.

**Wajumbe wa Yesu** ni chama cha wasichana na wavulana ambao ni wa umri wa miaka tisa na zaidi. Ni kazi ya wanawake wa kanisa kuongoza na kuwafundisha wasichana. Wasichana wanaweza kugawanywa katika makundi mawili, kundi moja kwa wasichana wadogo wenye umri wa miaka kutokea tisa mpaka kumi na mbili, na kundi moja lingine kwa wasichana wakubwa wa umri wa miaka kutokea kumi na mitatu mpaka watakapoolewa.

Makundi ya wavulana ya **Wajumbe wa Yesu** yanapaswa kuongozwa na wanaume wa Kibatisti. Wavulana wanaweza kugawanywa katika makundi mawili, kundi moja la wavulana

wadogo wa umri wa miaka 9-12, na kundi lingine kwa wavulana wakubwa. Wanawake wanaweza kuyatia moyo makanisa yao kukianzisha chama hiki cha wavulana. Wanaweza vile vile kuwatia moyo watoto wao kuwa washiriki.

## UHUSIANO WA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI NA KANISA

Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili ni sehemu muhimu ya kanisa. 'Inaubidi Ushirika huu kufanya kazi pamoja na kanisa na kulisaidia kanisa katika kila njia iwezayo kuendeleza kazi ya uenezaji wa injili kati ya washiriki wa kanisa. Inaupasa ushirika huu kusaidia katika elimu ya Ukristo kwa vijana wa kanisa katika vyama vyake vya vijana. Ushirika utayarishe ripoti mara moja kila mwaka kwa kanisa kuhusu kazi iliyofanywa na vyama vya wanawake na wasichana. Wanachama wa Ushirika watoe sadaka zao na kazi yao kusaidia katika kazi ya kanisa.

## SABABU YA KANISA KUWA NA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

Kila kanisa la Kibatisti limetiwa moyo katika kuanzisha Ushirika wa Wanawake Waenezao Injili. Wanawake hukutana mara moja kila wiki, kusoma mipango iliyotayarishwa na kuomba pamoja.

Hapa kuna sababu za kila kanisa la Kibatisti kuwa na chama hiki:

* Kazi ya kueneza injili ni kazi yetu. Kila mmoja wetu amepewa kazi ya kwenda ko kote ulimwenguni na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe. Watu hawawezi kwenda ikiwa hawajui. Hawataomba wala kutoa wala kumtumikia Mungu. Kwa hiyo watu wetu ni lazima wafundishwe maandiko kuhusu kulieneza Neno. Macho yao yanapaswa kufunuliwa kuona na mioyo yao kusikia mahitaji kwa injili kila mahali. Ni lazima waongozwe kutazamia kazi yao ya

kwenda kushuhudia nyumbani au katika nchi ya mbali. Ikiwa Mungu hawaiti kwenda katika nchi ya mbali, wanapaswa kusaidia kwa njia ya maombi yao na sadaka.

* Chama hiki cha Ushirika wa Wanawake hutoa mafunzo ya uenezaji kwa kusoma habari za kueneza injili katika Biblia na katika nchi mbalimbali.

* Ushirika wa Wanawake hufundisha mambo ya uwakili na kuishi kwa njia ya Kikristo.

* Ushirika wa Wanawake hutoa mafundisho kuwafundisha wasichana wote wa kanisa.

## VILE UNAVYOWEZA KUANZISHA USHIRIKA WA WANAWAKE WAENEZAO INJILI

Wanawake ambao wana hamu ya kuanzisha Ushirika wa Wanawake katika kanisa au katika kituo cha kuhubiri wafanye hivi:

* Zungumza na mchungaji na wanawake wengine katika kanisa juu ya kuanzisha kundi.

* Karibisha mmisheni mshauri kuja, kueleza kusudi la chama. Ikiwa hataweza kuja, pengine mwanamke mwingine kutoka katika kanisa lingine ambalo lina chama aweza kusaidia.

* Agiza vitabu, *Mipango ya Shirika Mpya,* kutoka Baptist Publications House, Box 30370, Nairobi. Agiza vya kutosha ili kila mwanamke awe na kitabu. Mipango iliyoko katika kitabu inaweza kila mwanamke awe na kitabu. Mipango iliyoko katika kitabu kutumika kila juma kwa miezi mitatu.

* Agiza nakala tatu za *Kitabu cha Maelezo* ya Umoja wa Wanawake Waenezao Injili kwa viongozi. Agiza nakala moja ya *Kitabu cha Ripoti.* Bei ya vitabu hivi iko katika orodha ya bei ya vitabu kutoka Baptist Publications.

* Tangaza mkutano wa kwanza. Karibisha wanawake wote wa kanisa na wanawake wengine ambao unataka kuwavuta kwa Mwokozi.

* Chagua Mwenye Kiti, Mwenye Kiti wa Mpango, na Karani.

* Viongozi wanahitaji kujifunza *Kitabu cha Maelezo* ili kwamba wajue kazi yao na kuongoza wanawake wengine.


* Baada ya kumaliza *Mipango ya Shirika Mpya,* agiza *IWE NURU* kwa kutumia kwa mikutano yako ya kila juma.

*Sura ya Pili*

# SHABAHA ZETU NA VILE TUNAVYOZIFIKIA

Ili tufanye kazi nzuri ni lazima tuwe na shabaha na mipango ya kazi. Shabaha zetu zinaelezwa katika sura hii. Maelezo yameandikwa pia ya njia ambazo tunaweza kufikia shabaha hizi.

## 1. KUPATA UFAHAMU



**Tutajaribu kuwa na ufahamu wa watu wote na kuwahurumia wale ambao wamepotea bila Kristo. Tutajaribu pia kuwa na ufahamu wa kazi yetu kama wanawake Wakristo. Tutaendelea kufanya mambo haya kwa kujifunza Biblia na kwa mafunzo yetu katika 'Iwe Nuru' na vitabu vingine vya Kikristo.**

Ni lazima tujue na kufahamu kabla ya kuweza kufanya. Ufahamu ndio hatua ya kwanza katika kutenda kwa Mkristo. Tunaweza kupata ufahamu kwa njia nyingi mbalimbali. Hapa kuna baadhi ya njia hizo:-

* Kuwa na mipango katika mikutano yetu itakayotusaidia kufahamu kazi zetu na mahitaji ya watu waliopotea katika sehemu zote za dunia. Mipango yetu yaweza kupatikana katika kitabu chetu, *Iwe Nuru.* Inatupasa kufikiria kukutana kila juma kwa mipango. Mipango itakuwa na maana kubwa ikiwa itatolewa kwa njia

mbalimbali na ikiwa matayarisho mazuri yamefanywa hapo mbeleni.

* Kuwa na somo la Biblia katika kila mkutano. Watie moyo washiriki wako kusoma Biblia kila siku.

* Watie moyo washiriki wote kuhudhuria Shule ya Jumapili na madarasa ya Biblia katika kanisa.

* Weka wakati kanisani, katika jumuiya, na katika Kusanyiko la Wabatisti kwa viongozi kujifunza kazi yao.

* Jaribu kuandika wanawake wote Wabatisti ili kwamba wote wajifunze pamoja.

Wakati mwingine kunaweza kuwa na washiriki wengine ambao hawakupata nafasi ya kwenda shuleni. Kwa kuwasaidia wanawake hao kuwa na ufahamu tunaweza kufanya mambo haya:-

* Watie moyo kuhudhuria madarasa ya kusoma na kuandika au wawe na madarasa maalum kuwasaidia kujifunza kusoma. Kutawawezesha kusoma Neno la Mungu na kuelewa.

* Kuwa na mafundisho maalum mara kwa mara juu ya afya nzuri, kutunza watoto, kupika, au hata kushona ili kwamba wanawake hawa Wakristo waweze kufahamu vizuri vile wanavyoweza kutimiza wajibu wao. Mmoja wa washiriki anaweza kufundisha mafundisho hayo maalum au mtu mwingine anaweza kualikwa kufundisha. Wanaohudhuria inawapasa kuelewa ya kwamba watalipa malipo ya vitabu na vitu vinginevyo vitakavyotumiwa.

Ni kazi ya Mwenye Kiti wa ushirika kuhakikisha ya kwamba mikutano hukutanika kila juma na ya kwamba Biblia hutumika katika mikutano. Mwenye kiti atataka kuona ya kwamba kuna nakala za kutosha za *Iwe Nuru* kwa mpango. Itakuwa kazi yake kuandika wanawake Wabatisti. Atakata shauri juu ya madarasa

maalum na mafundisho ya uongozaji. Atawatia moyo washiriki kusoma Biblia zao nyumbani.

Mwenye Kiti wa mpango atatengeneza mipango ya *Iwe Nuru* kwa mkutano wa kila juma.

## 2. KUKUA KATIKA MAISHA YA KIROHO



**Tutajaribu kutia nguvu maisha ya kiroho ya washiriki kwa kuwavutia kuomba na kujifunza Biblia katika mikutano yetu, nyumbani, na katika maisha ya binafsi.**

Maombi na uenezaji ya injili hayawezi kutenganishwa. Ni maombi na ushirika na Mungu ambazo huleta watu kumjua Mungu na kufanya kazi yake. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuendelea kuomba ili wajitayarishe kuja kwake Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste. Mpaka walipopokea Roho Mtakatifu hawakuweza kuwaleta watu 3,000 kwa Kristo.

Maombi yamehusika na kila sehemu ya kazi ya Ushirika wa Wanawake. Tunapokuwa na ufahamu wa mahitaji ya wengine katika mipango, tutaongozwa kuombea mahitaji haya. Tutataka kumwombea mchungaji wetu na ya kwamba wachungaji wengine wataitwa kufanya kazi katika Afrika ya Mashariki. Tutaombea shule za Kibatisti na hospitali yetu. Tutaomba kwamba makanisa ya Kibatisti yatafuata mafundisho ya Agano Jipya. Tutaombea taifa letu. Tutawaombea Wakristo wengine ko kote ulimwenguni na kazi yao kuvuta wale ambao wamepotea. Ushuhuda wa Kikristo hupata nguvu katika maombi.

Tufanye mambo haya ili tufikie shabaha yetu ya kukua katika maisha ya kiroho:

* Omba pamoja katika mikutano yetu. Mwombee kila mshiriki na mahitaji yake. Omba kwa ajili ya kundi letu na kazi yake.

* Omba na kusoma Biblia pamoja na jamaa zetu kila siku. Chagua saa nzuri kwa maombi haya ili kila mshiriki wa jamaa aweze kuwako.

* Omba na kusoma Biblia kila mmoja peke yake kila siku. Omba kwa nafsi yako ili ukue katika upendo na utumishi. Omba kwa ajili ya Bwana na watoto wako. Waombee wale unaojaribu kuwaleta kwa Kristo.

* Omba kwa uongozi wa Mungu kabla ya kwenda nje kushuhudia.

* Hudhuria ibada yote ya kanisa lako.

* Timiza Nyakati zetu maalum za Maombi. Tuna nyakati tatu maalum za maombi kila mwaka katika Umoja wa Wanawake. (a) Kila mwezi wa Machi tutaomba pamoja na wanawake wengine wa Afrika ya Mashariki kwa ajili ya watu wa nchi yetu na dunia nzima ambao wamepotea. Juma moja litatengwa kwa maombi. Mipango maalum itachapwa na sadaka zitakusanywa kusaidia kazi ya kutangaza neno la Mungu. Wakati huo utajulikana kama **Juma la Maombi.** Kila ushirika ukutane mara tatu bila kukosa katika juma hilo. (b) Kila mwaka tutaungana pamoja na wanawake wengine Wabatisti wa dunia nzima kwa maombi katika Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa Novemba. Hii ndiyo **Siku ya Maombi.**

Mwenye Kiti wa Mpango atatayarisha mipango maalum ya maombi.

## 3. KUWA MASHAHIDI WAKRISTO



**Tutajaribu kuwaongoza washiriki kuwa mashahidi Wakristo kwa ushuhuda wa Kristo kwa waliopotea na utumishi wa jamii inayoonyesha upendo wa Kristo. Tutajitahidi kutia nguvu maisha ya Kikristo nyumbani na katika jamii.**

Tu wafanya kazi pamoja na Mungu. Sisi wanawake Wakristo tuna neno la Mungu moyoni mwetu. Ni kusudi la Mungu sisi tuwe na sehemu katika kazi yake ya ukombozi. Katika jamii yetu au kijiji tutafute njia za kuwaleta wengine kwa Kristo au kufanya kazi kuonyesha upendo wa Ukristo.

Katika Ushirika wa Wanawake tunaiita kazi hii 'Utumishi wa Jamii.' Ni kazi ya kushuhudia juu ya Yesu Kristo na kusaidia watu wengine. Kazi hii imepangwa kwa kusudi la kuwaleta watu kwa Kristo ambao bado hawajaokolewa na kufanya mahali pa jirani wetu kuwa mahali pa watu kuishi kama Kristo.

Kila ushirika upange kazi ya kufanya kila mwezi. Mwenye Kiti aongoze kundi kutengeneza mpango wa kazi hii. Mipango hii iandikwe katika *Kitabu cha Ripoti* na mwandishi katika ukurasa ambapo umeandikwa maneno 'Utumishi wa Jamii.' Ikiwa makundi yanataka kupanga zaidi ya kazi moja kila mwezi, ni vizuri zaidi. Kila mshiriki anahimizwa kufanya mengi kama awezavyo.

Hapa kuna mawazo juu ya kazi ambazo vikundi vinavyoweza kufanya:-

* Tembelea watu waliopotea. Wawili watatu waende pamoja. Zungumza juu ya uhitaji wao wa wokovu na vile wanavyoweza kuwa nao.

* Ongoza ibada au maombi katika gereza, mahospitalini, au mahali pengine ambapo hapana makanisa. Kila mara uwe na ruhusa kutoka kwa wasimamizi wa kazi hii kabla ya kuongoza mikutano hiyo maalum.

* Soma maneno ya Mungu kwa wale ambao hawawezi kusoma. Wafundishe vifungu vya Biblia.

* Fundisha wengine kusoma Biblia.

* Tembelea nyumba za walio wagonjwa na wazee. Wasomee Neno la Mungu.

* Toa vijitabu vidogo, masomo ya Shule ya Jumapili, na vifungu vya Biblia kwa wengine kusoma na kujifunza juu ya njia za Kikristo.

* Walete marafiki, majirani, na jamaa yako kanisani pamoja nawe.

* Rembesha kiwanja cha kanisa na usaidie kuweka kanisa likiwa safi na lenye kuvutia. Panda maua nje na weka maua kanisani kila Jumapili.

* Ikiwa kuna kifo katika jamaa ya mtu ambaye hajaamini, mtembelee mtu huyo, Mwambie juu ya upendo wa Mwokozi na huruma yake wakati wa huzuni.

* Iwapo mtoto amezaliwa, tembelea mamake. Mwambie vile Yesu anavyowapenda watoto wadogo. Mkaribishe kuja kanisani ili ajifunze juu ya Yesu na kuweza kumfundisha mtoto wake.

* Uwe na madarasa ya kusoma, kushona, au kupika katika mahali ambapo hapana kanisa la Kibatisti. Soma Biblia katika mikutano. Fanya haya ili uwavute wanawake kwa Kristo.

* Saidia kuanzisha Ushirika wa Wanawake katika kanisa lingine karibu ambalo halijaanza bado ushirika huu. Enenda

kanisani na kufundisha wanawake wa kanisa kusudi lake na vile wanavyoweza kukutana. Nenda katika mikutano yao kwa kawaida mpaka watakapoweza kuongoza mikutano yao wenyewe.

* Tembelea Wakristo na washiriki wa kanisa ambao hawana bidii katika kanisa na kuwatilia moyo kuhudhuria ibada ya kanisa.

* Saidia wenye shida kwa kuwapelekea chakula, kusaidia kuangalia watoto, au kusaidia kazi za nyumbani. Fanya yote katika roho ya upendo na usaidizi.

* Uwe na michezo katika kiwanja cha kanisa kwa vijana.

* Onyesha mfano mzuri wa kukumbuka Siku ya Bwana.

## 4. KUSHIRIKI MALI YETU



**Tutajaribu kuendeleza Wakristo kushiriki kwa njia ya kufundisha uwakili. Tutawatia moyo washiriki kutoa fungu la kumi na kutoa sadaka maalum kupeleka neno la Mungu katika sehemu zingine za nchi yetu au dunia.**

Uwakili ni kutoa wakati wetu, uwezo wetu na pesa zetu pamoja na maisha yetu kwa Yesu. Hii ni mipango yetu kwa kutoa na uwakili:-

* Kila mshiriki anahimizwa kupata mali yake kwa njia ya haki.

* Kila mshiriki inampasa kutoa fungu la kumi na vitu vyake kwa kanisa kama inavyofundishwa katika Biblia. Hii haitatolewa katika mikutano ya Ushirika wa Wanawake, lakini itolewe Jumapili katika kanisa. Ikiwa mwanamke hutoa fungu lake la kumi kanisani

kwa kawaida, mwandishi ataweka alama kando ya jina lake ndani ya *Kitabu cha Ripoti* kuonyesha yeye ni mwenye kutoa fungu la kumi.

* Kila mshiriki atumie vitu vyake kwa njia ambayo itamtukuza Mungu.

* Sadaka maalum hutolewa katika Juma la Maombi katika mwezi wa Juni kusaidia kutangaza Injili katika Afrika ya Mashariki au nchi zingine. Hutangazwa kila mwaka kazi ambayo sadaka hizo zitasaidia.


* Sadaka maalum hukusanywa Siku ya Maombi katika Mwezi wa Novemba kuendesha Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Afrika nzima na kazi yake ya kusaidia.

* Sadaka zote maalum za Kenya hutumwa katika afisi ya **Umoja wa Wanawake, Box 30514, Nairobi, Kenya.** Sadaka maalum za Tanzania zipelekwe kwa anwani ambayo imetangazwa.


* Sadaka inaweza kutolewa katika kila mkutano kwa kusudi lo lote ambalo kundi litachagua. Kuna mahali katika upande wa chine wa kila ukurasa katika *Kitabu cha Ripoti* kuandika kiasi cha sadaka zilizopokewa katika kila mkutano.

* Karani ataweka orodha nzuri ya pesa zote ambazo zimepokewa na zile ambazo zimetumiwa. Atakuwa akitangaza kwa kawaida kwa kundi juu ya pesa ambazo zimewekwa, kiasi cha pesa ambazo ni za sadaka maalum, na namba ya wetu wanaotoa fungu la kumi.

## 5. KUFUNDISHA WATOTO NA VIJANA



**Tutajaribu kufundisha watoto wetu na wengine juu ya Mwokozi wetu. Tutajitahidi kuongoza watoto na vijana kufahamu habari ya Kristo katika vyama vinavyokutana katika siku za juma katika makanisa yetu.**



Mama Mkristo ana madaraka ya kufundisha watoto wake juu ya Mungu. (Soma Kumbukumbu la Torati 6:4-7 na Mithali 22:6.) Vile vile wanawake wa kanisa wana madaraka ya kuwafundisha watoto wa kanisa. Kwa sababu tunataka watoto hawa na wengine kuwa na mafundisho ya Kikristo, tutawaleta katika Shule ya Jumapili.

Tunaweza pia kuanzisha "Wajumbe wa Yesu" kwa wasichana. "Wajumbe wa Yesu" ni chama cha wasichana walio na umri wa miaka minane na zaidi. Wasichana ndio walio na madaraka ya wanawake. Ikiwezekana ni vizuri kuwa na vyama viwili vya wasichana, moja kwa wasichana wadogo na kingine kwa wasichana walio na umri wa zaidi ya miaka kumi na miwili.

Kwa sababu wanawake wanataka wavulana wao kuwa na mafundisho ya Kikristo pia, wengine wanataka wavulana wadogo kushirikiana na wasichana katika chama cha "Wajumbe wa Yesu". Wengine wanaanzisha "Wajumbe wa Yesu" hasa kwa wavulana wadogo.

Kiongozi wa "Wajumbe wa Yesu" anahitaji kitabu cha "Maongozi ya Mshauri" ili ajue njia ya kuongoza na kuendesha mikutano. Akiweza kujifunza kazi ya "Wajumbe wa Yesu" katika semina ya viongozi ataweza kufanya kazi yake vizuri mno.

Kiongozi atahitaji kitabu cha "Ujumbe" kutumia katika mikutano. Somo la kila wiki linapatikana katika "Ujumbe".

Kila mshiriki, msichana au mvulana, atahitaji, "Kitabu cha Mshiriki." Kitabu hiki kinaeleza kazi ya kufanya na vifungu vya kujifunza.

Mkitaka kuanzisha "Wajumbe wa Yesu," mfuateni hatua hizi:

1. *Chagua viongozi.* Chagua wanawake ambao ni washiriki wa "Ushirika wa Wanawake." Mkishindwa kupata mama awezaye kuongoza, tafuta msichana ambaye amekomaa na ni mshiriki mwaminifu wa kanisa lenu.

2. *Nunua vitabu.* Kila Mshauri atahitaji vitabu hivi: "Maongozi ya Mshauri" na "Ujumbe." Kila mshiriki atahitaji, "Kitabu cha Mshiriki." Vitabu hivi vinapatikana kutoka Baptist Publications, Box 30370, Nairobi, Kenya, au Baptist Literature Centre, S.L.P. 1240, Moshi, Tanzania.

3. *Washauri wajifunze kazi yao.* Wanaweza kujifunza katika semina au kwa kusoma vitabu vya "Wajumbe wa Yesu" vinavyotajwa katika Nambari 2, au wanaweza kutembelea mikutano ya "Wajumbe wa Yesu" katika kanisa lingine na kuona jinsi wafanyavyo.

4. Chagua siku ya mkutano wa kwanza na mahali.

5. Tangaza mkutano katika Shule ya Jumapili na ibada ya kanisa. Wakaribishe wasichana wote kuhudhuria. Ukitaka wavulana kujiunga, wakaribishe wavulana pia.

6. Kutana kila wiki.

7. Omba uongozi wa Mungu wakati wote.

Katika mkutano mshauri atafundisha somo kutoka "Ujumbe." Masomo ni juu ya Biblia, au kazi ya Wabatisti katika nchi mbalimbali, au maisha ya Mkristo. Baada ya mpango vijana wanaweza kucheza michezo au kufanya kazi ya mikono.

Mara kwa mara Wajumbe watajifunza vifungu vya Biblia na mambo mengine. Mpango huu wa kujifunza huitwa "Hatua za Maendeleo." Anapomaliza kila hatua, msichana atapewa beji kuonyesha maendeleo yake.

Wanawake wote wa Ushirika wanaweza kusaidia kwa njia-hizi:

* Kuwakaribisha wasichana kuhudhuria mikutano.


* Kusaidia kununua vitabu na vitu vingine ambavyo vitatumika katika mikutano.

* Kusaidia kwa michezo au kazi ya mikono ikiwa kuna wasichana wengi.

* Kufanya kazi katika kamati ambayo husikiza yanayosemwa na wasichana kutoka vichwani mwao bila kusoma, (yaani, Hatua za Maendeleo) kuhakikisha ya kwamba wamefanya kazi yao vizuri.

Mwanamke ambaye ni kiongozi apaswa kutoa ripoti kwa Ushirika wa Wanawake juu ya maendeleo ya wasichana. Inampasa pia kuweka orodha ya wasichana ambao walihudhuria.

# VIONGOZI NA WASHIRIKI NA KAZI YAO



Viongozi wa kweli huongoza chama chao kwendelea mbele. Bila viongozi wazuri chama kitakuwa nyuma.

Viongozi wa Ushirika wa Wanawake wachaguliwe kila mwaka. Ni vizuri kuwachagua katika mwanzo wa mwaka. Ikiwa mmoja amefanya kazi nzuri, labda washiriki watapenda kumchagua tena, lakini wanaweza kumchagua mtu mwingine ikiwa wanapenda. Kabla ya kuchagua viongozi omba kwa uongozi wa Mungu.

Kuna mambo muhimu ambayo viongozi wanapaswa kuwa nayo:

* Ni lazima wawe Wakristo wazuri.

* Ni lazima wawe washiriki waaminifu wa Kanisa la Kibatisti.

* Ni lazima wawe tayari kufanya kazi na kuitayarisha vizuri.

* Ni lazima wawe wenye maamuzi mazuri na kuchagua kwa akili katika mambo yote.

* Ni lazima wawe na upendo na ujuzi kuelekea watu wa makabila na mataifa yote.

* Ni lazima wajitoe kwa kutangaza Neno la Mungu duniani mwote.

* Ni lazima wawe wenye kupenda kujifunza. Wanaweza kuwa na ujuzi wa kazi yao kwa kujifunza kitabu hiki na kwa kuhudhuria mikutano ya Jumuiya na mafundisho mengine.

Hawa ni viongozi ambao hata chama kidogo kinaweza kuwa nao:-

MWENYE KITI
MWENYE KITI WA MPANGO
KARANI

Ikiwa una wanawake wa kutosha ambao wanaweza kusoma, labda utataka kugawanya madarasa ya viongozi hawa ili kwamba wanawake wengi watakuwa na nafasi ya kusaidia.

Kazi ya viongozi imeelezwa hapa chini.

## MWENYE KITI

1. Ataongoza mikutano yote. Mwenye Kiti anapoongoza, inampasa kusimama mahali ambapo wote wanaweza kumwona na kumsikia. Huenda atapendezwa kufuata utaratibu wa ibada hii au ule wa mpango wa kila juma wa *Iwe Nuru.*

**Wimbo** (Chagua nyimbo kabla ya mkutano haujaanza.)
**Maandiko:** (Mwenye Kiti anaweza kusoma au kumwuuliza mtu mwingine kufanya hivyo.)
**Maombi**
**Sadaka**
**Kuita Majina** (Karani anaweza kufanya mambo haya.)
**Ripoti ya Pesa**
**Mipango ya Utumishi wa Jamii** (Mwenye Kiti ataongoza kundi kwa kutayarisha kazi hii ya kushuhudia na kutumika.)
**Ripoti Nyingine na Shughuli**
**Matangazo**

**Mpango** (Mwenye Kiti wa Mpango ataongoza kwa kipindi hiki.)

**Maombi ya Kufunga**

1. Huongoza shughuli za chama.

3. Huandikisha wanawake wote wa Kibatisti.

4. Hupanga mpango wa utumishi wa jamii na kuongoza kundi katika kazi hii.

5. Husaidia viongozi kujifunza kazi yao kwa kujifunza *Kitabu cha Maelezo* au kwa kuhudhuria mikutano katika Jumuiya.

6. Hutengeneza ripoti ya mwaka pamoja na karani na kuituma kwa **Umoja wa Wanawake, Baptist Publications, Box 30370, Nairobi, Kenya.** Katika Tanzania ripoti itumwe kwa anwani inayotangazwa.

## MWENYE KITI WA MPANGO

1. Hutayarisha mpango kwa kila mkutano kutoka *'Iwe Nuru'*. Hutoa sehemu mbeleni ili wale watakaosoma watajiweka tayari. Hutumia washiriki wengi mbalimbali kwa kutoa mpango. Hupanga njia tofauti za kutoa mpango. Hapa kuna mambo fulani anayoweza kufanya ili mpango uwe wa kuvutia:-

* Uliza kila mmoja kueleza sehemu yake badala ya kusoma.

* Uliza maswali juu ya mpango.

- Uwe na mchezo wa kujulisha habari katika mpango.

* Wakati mwingine mgeni anaweza kukaribishwa kusema juu ya kiini cha mpango.

* Tumia picha, ramani, au kitu kitakacho wasaidia washiriki kuelewa maana ya mpango.

2. Hupanga Mpango wa Maombi. Hutafuta kufanya mipango hii kuwa wakati halisi wa maombi. Hutumia mawazo haya juu kumsaidia.

3. Huongoza ikiwa Mwenye Kiti hayuko.

## KARANI

1. Huandika orodha ya majina ya washiriki wote.

2. Huweka *Kitabu cha Ripoti* kwa njia nzuri. Huandika majina ya viongozi na washiriki. Huonyesha katika nafasi zilizotayarishwa kwa kazi hii ikiwa washiriki wamebatizwa na ikiwa hutoa fungu la kumi. Huandika jumla ya waliohudhuria kila juma na jumla ya sadaka. Huandika kila mwezi kazi ambayo kundi litafanya kwa Utumishi wa Jamii. Hutumia kurasa ambazo zina mistari peke yake kuongeza jumla ya sadaka au kuandika shughuli nyingine.

3. Huweka hesabu za sadaka zote na kuonyesha vile pesa zimetumika.

4. Hutoa ripoti kwa kundi kwa kawaida juu ya hesabu ya wanachama na juu ya pesa.

5. Husaidia Mwenye Kiti kutengeneza ripoti ya kila mwaka katika kurasa za mwisho katika *Kitabu cha Ripoti*. Nakala moja ya ripoti hii hupelekwa kwa **Umoja wa Wanawake, Baptist Publications, Box 30370, Nairobi, Kenya.** Katika Tanzania ripoti itumwe kwa anwani inayotangazwa. Nakala ile nyingine huachwa katika kitabu ili isomwe kwa kanisa na jumuiya.

6. Hupeleka sadaka maalum kwa anwani ambayo imeonyeshwa katika mpango.

7. Huwavuta wanawake kuwa mawakili wema.

## VIONGOZI WENGINE NA KAMATI

Ikiwa una washiriki wengi, unaweza kugawanya madaraka ya viongozi. Unaweza kuchagua makamu kwa kila kiongozi. Unaweza kugawanya kazi ya karani na kuchagua mwanamke mmoja kuwa mwandishi na mwingine kuwa mweka hazina. Unaweza kuchagua Mwenye Kiti wa Utumishi wa Jamii, Mwenye Kiti wa wanachama, Mwenye Kiti wa Uwakili, Mwenye Kiti wa Maombi, na Kiongozi wa wasichana.

## WASHIRIKI WETU NA MADARAKA YAO

Kila mshiriki mwema wa Ushirika wa Wanawake anajua ya kwamba ana kazi ya kufanya pia. Huhudhuria kwa uaminifu. Hujaribu kuandika wanawake wengine Wabatisti. Husoma sehemu ya mpango. Huomba pamoja na wanawake wengine na ataongoza maombi ikiwa ameulizwa. Huwa na sehemu katika Utumishi wa Jamii. Hutumika katika kamati ikiwa ameulizwa kufanya hivyo. Hujaribu kuwa wakili mwema. Ebu na tusisahau kwamba 'Tu wafanya kazi pamoja na Mungu.' Kila mwanamke ana kazi ya kufanya.

# WANAWAKE WABATISTI WAJIUNGA PAMOJA

Wanawake wa Kibatisti huongezewa nguvu kwa kukutana pamoja kwa ushirika na mafunzo. Kwa kujiunga pamoja wanaweza kuzidisha bidii zao kwa maombi, kwa kujifunza Biblia, kutoa mali zao, na kutumika.

## JUMUIYA

Wanawake wa Kibatisti katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki wameanzisha jumuiya. Jumuiya hizi zimefanywa na wajumbe kutoka Shirika za Wanawake mbalimbali kutoka katika makanisa ya Kibatisti katika mahali hapo. Huchagua viongozi na kukutana pamoja kwa maongozi ya Mungu, mafunzo na ushirika.

Hapa kuna maelezo ya kukusaidia kwa kutayarisha kazi ya Umoja wa Wanawake Waenezao Injili wa jumuiya yako.

### 1. VIONGOZI

* Kila jumuiya ichague viongozi wafuatao:-

MWENYE KITI
MWENYE KITI MDOGO
MWANDISHI
MWEKA HAZINA

* Ikiwa jumuiya inataka, wanaweza kuchagua Kiongozi wa nyimbo, Mwneye Kiti wa Vijana, na viongozi wengine.

* Katika jumuiya kubwa wajumbe kutoka wilaya mbalimbali wanaweza kuchaguliwa.

* Kazi ya viongozi itakuwa kama ifuatavyo:-

**MWENYE KITI**

Huongoza mikutano yote.

Hujishughulisha na shughuli za Umoja wa Wanawake Waenezao Injili wa Jumuiya.

Huyahimiza makanisa kuwa na shirika na kusaidia kuzianzisha.

Yeye ndiye anayeongoza kazi maalum za Umoja wa Wanawake Waenezao Injili wa Jumuiya.

Huwasimamia wanawake katika mikutano ya Jumuiya nzima.

**MWENYE KITI MDOGO**

Hutengeneza mipango ya mikutano.

Huongoza ikiwa Mwenye Kiti hawezi kuhudhuria.

**MWANDISHI**

Huweka orodha ya shirika zote na mahudhurio yao katika mikutano.

Huandika muhtasari wa mambo makuu ya mikutano.

**MWEKA HAZINA**

Huweka mpango wa pesa zote ambazo zimepokewa na zile ambazo zimetumika.

Hutoa ripoti katika kila mkutano.

**2. MIKUTANO**

* Kila jumuiya ijaribu kuwa na mikutano miwili kila mwaka.

* Mikutano mingi inaweza kukutanika ikiwa jumuiya inataka.

### 3. MAHUDHURIO

* Wajumbe kutoka shirika ambazo zimeundwa katika makanisa wanaweza kuhudhuria mikutano. Wajumbe wanaweza kuchaguliwa kwa njia yo yote ambayo jumuiya inataka.

* Wageni kutoka makanisa yasio na shirika wanaweza kuhudhuria ikiwa jumuiya inataka.

### 4. MATUMIZI

* Jumuiya pamoja na mshauri mmisheni katika sehemu ile wakate shauri juu ya njia ya kulipa bei ya matumizi ya chakula, kusafiri, na mipango.

### 5. MPANGO

* Mpango kwa mikutano itayarishwe na viongozi pamoja na mmisheni mshauri. Kujifunza Biblia na mahubiri ya kuvuta watu kwa Mungu yawekwe katika mpango pamoja na mafunzo ya afya au njia ya kutunza watoto na vile iwezekanavyo kuwa na Ushirika wa Wanawake wema. Maoni ya mipango ya Umoja wa Wanawake wa Jumuiya yanaweza kuongezewa katika Makusanyiko ya Wabatisti.

### 6. KAZI

* Jumuiya inaweza kuchagua kazi ambayo itakayofanya kushuhudia juu ya Kristo, kusaidia watu, au kutumia makanisa ya Kibatisti. Kazi yo yote ambayo itakayochaguliwa iwe kazi ambayo kila ushirika unaweza kusaidia kwa kutoa au kwa kutumikia.

## JUMUIYA KUU YA WABATISTI

Wabatisti wa nchi moja hupenda kujiunga pamoja ili waeneze injili katika taifa lao na kushirikiana na makanisa mengine yenye imani ya Kibatisti. Wanawake husaidia kazi ya Jumuiya Kuu katika

nchi yao kwa kuomba na kutoa sadaka zao. Idara ya wanawake hukutana mara kwa mara kupanga kazi yao na kujifunza pamoja na dada zao.

Katika Kenya Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Kenya Waenezao Injili hukutana kila mwaka. Wanawake kutoka makanisa yote wanaweza kuhudhuria. Kila Jumuiya Ndogo inaweza kumtuma mjumbe kwa mikutano ya Kamati Kuu.

Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Tanzania Waenezao Injili hukutana kila miaka mitatu. Miaka mingine wanawake wa eneo moja wanakutana.

## UMOJA WA WANAWAKE WABATISTI WA BARA AFRIKA

Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Bara Afrika umeundwa na wajumbe kutoka makundi ya wanawake katika nchi zote za Afrika pale ambapo pana kazi ya Wabatisti. Umoja huu hukutana baada ya kila miaka mitano. Ndio kiungo cha kutuunganisha sisi, na wanawake Wabatisti katika Afrika na pande zote za dunia.

Kusudi la Umoja ni:-

* Kuendeleza ushirika mwema, kuwa na huruma kubwa, na ufahamu kamili kati ya Wanawake wa Kibatisti wa Afrika.

* Kuwatia moyo wanawake kuungana pamoja kwa utumishi wa Kikristo.

* Kuungana pamoja na wanawake wengine Wabatisti wa dunia katika Siku ya Maombi.

Sadaka ambazo tunapokea Siku ya Maombi husaidia umoja huo na kazi yake ya msaada katika bara ya Afrika.

Gazeti liitwalo *The Organ of News* huchapwa kwa Kiingereza mara mbili kwa mwaka kuleta habari kutoka nchi mbalimbali.

Nakala za gazeti ni bure zikiagizwa kutoka afisi ya Umoja wa Wanawake, Nairobi, au afisi ya wanawake katika Tanzania.

## BAPTIST WORLD ALLIANCE

Baptist World Alliance (Mwungano wa Wabatisti wa Ulimwengu) imefanywa na makundi ya Wabatisti kutoka pande zote za ulimwengu. Chama hiki kinakutana baada ya kila miaka mitano.

Mojawapo ya sehemu za Baptist World Alliance ni Idara ya Wanawake. Kuna Umoja wa Wanawake Wabatisti katika kila bara kuu, yaani tano. Tunahusika na Idara wa Wanawake kwa njia ya uanachama wetu katika Umoja wa Wanawake Wabatisti wa Bara Afrika. Siku ya Maombi ya Wanawake Wabatisti wa ulimwengu inatayarishwa na Idara ya Wanawake kila Jumatatu ya kwanza ya mwezi wa Novemba. Tunaungana na wanawake wa mataifa yote siku ile tukiomba pamoja.

## VIFUNGU VYA BIBLIA KUJIFUNZA NA KUKUMBUKA

(Ukiweza kusema kifungu kwa moyo, andika tarehe ulipojifunza kifungu.)

1. Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Warumi 3:23. ____________
2. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. Isaya 53:6. ____________

3. Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. Warumi 6:23 ______
4. Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. Mathayo 16:31 ______
5. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16 ______
6. Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Warumi 10:13 _
7. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu. Waefeso 2:8 ______
8. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. I Yohana 1:9 ______
9. Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Yohana 14:6 ______
10. Mkinipenda mtazishika amri zangu. Yohana 14:15 ______
11. Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Marko 16:15 ______
12. Mpende jirani yako kama nafsi yako. Marko 12:31 ______
13. Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, Dunia na wote wakaao ndani yake. Zaburi 24:1 ______
14. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja. I Kor. 16:2 ______
15. Ni heri kutoa kuliko kupokea. Matendo 20:35 ______
16. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao. Mathayo 18:20 _
17. Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Yohana 16:23 ______
18. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. Mathayo 6:33 ______
19. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. Wafilipi 4:13 ______

20. Mwanamke amchaye Bwana, ndiye atakayesifiwa. Mithali 31:30 ____________________

21. Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu. Zaburi 119:105 ____________________

22. Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. 1 Wakorintho 10:31 ________

23. Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu. Warumi 14:12 ____________

24. Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu. 1 Petro 1:16 ____________________

25. Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu. Yakobo 1:22 ____________________